

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO



**TAMKO LA MGENI RASMI KATIBU MKUU WIZARA YA AFYA,
MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO, PROF
MABULA MCHEMBE SIKU YA AFYA YA AKILI DUNIANI
TAREHE 10 OKTOBA 2020.**

Ndugu Wananchi,

Siku ya Afya ya Akili, huadhimishwa Duniani kote kila mwaka ifikapo tarehe 10 ya Mwezi Oktoba.

Kauli mbiu ya Maadhimisho ya Siku ya Afya ya Akili Duniani mwaka 2020 ni “ **Afya ya Akili kwa wote, Wekeza zaidi, Fikia huduma Zaidi** ” (Mental Health for All, greater Investment, Greater Access). Kauli Mbiu ya mwaka huu inalenga kuhamasisha Wananchi na jamii yote kwa ujumla kuelewa kuwa huduma ya Afya ya Akili ni haki ya kila mmoja wetu kuifikia, na kuwakumbusha watunga sera, serikali na wawekezaji kuhakikisha kuwa inawekeza zaidi katika miundo mbinu, watumishi wenye taaluma ya Afya ya Akili, Dawa na Vifaa Tiba, sera nzuri ili kuifanya jamii iweze kuifikia

huduma hii kwa usawa, na kiwango bora cha utlewaji wa huduma hii.

Aidha, tunakumbushwa wazazi, walezi, jamii na serikali za Mataifa Duniani katika kuwajibika na kuwalea vijana kuwa na maadili mema na kujiepusha na uvunjaji wa haki za binadamu, matumizi ya dawa za kulevya, makosa ya kimtandao na unyanyasaji wa kimtandao na ongezeko la matukio ya kujua (suicide).

Ndugu wananchi

Wataalam wa afya ya akili wanatukumbusha kuwa ili kuifanya Afya ya Akili ili iwe kwa wote inahitaji mambo mengi yakiwemo ya kibajeti, Rasilimali watu, na usawa wa usambazaji wa wataalam kwa kuzingatia jiografia ya nchi, mijini na vijijini.

Pia kuanzisha au kuimarisha vyo vilivyopo viwe na uwezo wa kudahili wanafunzi wengi ili kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa rasilimali watu katika maeneno mbalimbali ya nchi.

Ndugu wananchi

Takwimu za shirika la afya ulimwenguni zinaonesha kuwa takribani nusu ya magonjwa yote ya akili huanzia katika umri wa miaka 14 na kwa bahati mbaya vijana wengi wenye matatizo haya, hawapati nafasi ya kutambulika na kupatiwa matibabu katika wakati muafaka. Magonjwa ya akili na matumizi ya vilevi ni miongoni mwa changamoto kubwa sana za kiafya na kiusalama zinazoathiri jamii.

Kwa mfano, ugonjwa wa Sonona (Depression) unashika nafasi ya tatu kwa magonjwa yote yanayoathiri jamii. Pia kujiua (suicide) inaaminika ni chanzo kikuu cha pili cha vifo vyote vinavyowakabili jamii Duniani. Huku utumiaji wa mihadarati (dawa za kulevya) ukiwa ndio changamoto kubwa inayowakabili vijana katika mataifa yote. Utumiaji wa dawa za kulevya na pombe vimehusishwa kwa kiasi kikubwa na tabia hatarishi za ngono zembe na ajali za barabarani.

Ndugu Wananchi,

Takwimu zetu za mwaka 2015 kwa vijana wenye miaka 13 – 17 katika shule za msingi na sekondari katika mikoa 21 ya Tanzania Bara pia zinaonesha uwepo wa dalili za sonona (Depression) kwa zaidi ya asilimia 7 ya vijana waliohojiwa, huku asilimia 14 ya vijana wote wakiripoti mawazo ya kutaka kujiua (suicide ideation) na kati yao zaidi ya asilimia 11 wakijaribu kufanya hivyo.

Tatizo la pombe na sigara yaliripotiwa kwa kiwango sawa cha asilimia 5, huku asilimia 3.1 wakiripoti kuwa walishawahi kutumia bangi katika maisha yao. Aidha karibu robo ya vijana wote waliohojiwa waliripoti kufanyiwa uonevu (Bullied) na wenzao kwa kupigwa, kusukumwa au kufungwiwa madarasani.

Ndugu Wananchi,

Tunapozungumzia afya tunamaanisha hali ya ustawi wa mwanadamu kimwili, kiakili na kijamii. Mtu mwenye afya njema ya akili anaaminika kutengemaa katika namna anavyofikiri, anavyohisi, na anavyotambua mambo, ambayo kwa pamoja hujionyesha katika matendo yake ya kila siku ikiwa ni pamoja na jinsi anavyohusiana na kushirikiana na wenzake katika familia na jamii na shuleni ama mahali pa kazi.

Ndugu Wananchi

Katika kukabiliana na changamoto hizi, Tanzania kama zilivyo nchi zingine wanachama wa shirika la Afya Duniani wanaadhimisha siku hii, ambapo Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, waratibu wa Afya ya Akili na Wadau Mbalimbali wameandaa shughuli za kutoa elimu kuhusu umuhimu wa Afya ya Akili kwa wote, kuisitiza jamii kuwekeza zaidi katika Nyanja tofauti za huduma ya Afya ya Akili. Katika Kipindi cha Miaka Mitano iliyopita Serikali imepanua wigo wa udahili kwa wanafunzi wanaofanya Shahada ya uzamili kwenye Taaluma ya Afya ya Akili na kuongeza idadi ya Madaktari Bingwa wa Afya ya Akili, Wasaikolojia Tiba na watendaji wengine kwenye eneo hili la huduma ya Afya ya Akili. Sambamba na Ongezeko la wataalam Serikali imeongeza ushirikishwaji wa wadau kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo miundo mbinu, watumishi, rasilimali

fedha, dawa na vifaa tiba na mazingira wezeshi ya kufikia huduma za afya ya akili katika ngazi zote za kutolea huduma.

Katika kuhakikisha jamii inapata huduma bora za Afya ya Akili na Wizara ya Afya kwa Kushirikiana na Wadau itaendelea kutoa huduma za elimu ya Afya ya Akili kwa jamii kwa kulenga makundi maalum ambayo yapo kwenye uhatarishi zaidi. Makundi ya vijana yanaonekana kuwa na changamoto zaidi za afya ya akili katika ulimwengu wa mabadiliko hususani madhara ya matumizi ya dawa za kulevya, madhara ya kucheza kamali, unyanyasaji wa kimtandao na matukio ya kujiua.

Aidha, itaelimisha juu ya unyanyasaji wa vijana mashuleni, na majumbani ili kuwapunguzia au kuwakinga vijana kuwa katika hatari ya kupata magonjwa ya akili, kujiua au kuingia kwenye matumizi ya dawa za kulevya. Elimu itakayotolewa itawafanya walimu, wazazi, walezi na serikali kujua umuhimu wa kinga na huduma ya afya ya akili kwa jamii na maendeleo ya Taifa.

Sambamba na elimu kwa umma, wizara pia imekuwa ikitoa huduma za tiba za magonjwa ya akili na matumizi ya dawa za kulevya katika hospitali zote za umma nchini.

Pia uanzishwaji wa vituo vya kutoa huduma au matibabu ya kwa waathirika wa matumizi ya dawa za kulevya kwa njia ya methadone katika mikoa ya Dar es salaam, Mbeya, Mwanza na Dodoma ambavyo vimefikia 9 na kuwahudumia waathirika takribani 8500.

Pia serikali itaendelea kusimamia na kuboresha sera ya mwongozo wa afya ya akili ya mwaka, 2006 na Sheria ya afya ya akili ya mwaka 2008 na sera ya vijana. Vilevile kuimarisha huduma za afya ya akili katika ngazi ya Msingi, na kuhakikisha kila Mkoa unaimarisha huduma hizi Tanzania Bara na kuwajengea uwezo watoa huduma za afya ya Akili nchini ili waweze kutambua na kubaini mapema dalili za magonjwa ya akili na kutoa matibabu stahiki au rufaa kwa wakati muafaka.

Hata hivyo zipo changamoto mbalimbali katika utoaji huduma kwa wagonjwa wa afya ya akili nchini.

Ndugu Wananchi,

Dhamira kuu ya maadhimisho ya mwaka huu 2020, ni kuhakikisha afya ya akili inakuwa sehemu ya agenda ya kimkakati wa kuimarisha huduma Afya nchini. Hali kadhalika inalenga kuongeza thamani, heshima na utu wa mgonjwa wa akili, kuzionyesha huduma za afya ya akili kama sehemu muhimu ya huduma ya mwili wa binadamu, kupunguza unyanyapaa, kutengwa na kunyanyaswa, kuifanya jamii kuongeza uelewa na kutambua magonjwa ya akili kama magonjwa mengine na hasa kuyapa kipaumbele.

Ndugu Wananchi,

Serikali imeendelea na utekelezaji wa Sera ya Afya ya mwaka (2007) ambayo inalenga kutoa huduma bora kwa wagonjwa wa akili na magonjwa mengine yasiyo ambukiza.

mSerikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeendelea kutambua uwepo wa maadhimisho ya siku ya Afya ya Akili duniani kama sehemu ya uhamasishaji kwa jamii kama ilivyo kwenye nchi zote duniani.

Ndugu Wananchi,

Ili kuboresha hali ya afya ya akili Serikali kwa kushirikiana na wadau itahakikisha kwamba:-

(1) Watumishi wa afya wanapewa mafunzo maalum ya namna ya kuwahudumia wagonjwa wa akili na matatizo ya kisaikolojia kwa vijana na jamii kwa ujumla.

(2) Kufanya tafiti mbalimbali zinazosaidia kuboresha huduma za kuzuia na kudhibiti magonjwa ya akili katika jamii.



Prof. Mabula Mchembe

Katibu Mkuu

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii

Jinsia, Wazee na Watoto

10/10/2020